



# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS,  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



## HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. CAB.75/291/01/77

Tarehe: 10 Disemba, 2020

Wahe. Wabunge wa Kuchaguliwa,  
Wahe. Wabunge wa Viti Maalum,  
Wahe. Madiwani wa kuchaguliwa,  
Wahe. Madiwani wa Viti Maalum,  
Halmashauri za Manispaa za Mkoa wa Dar-es-salaam,  
**DAR ES SALAAM.**

Yah: WITO WA KUHUDHURIA MKUTANO WA MADIWANI WOTE  
UTAKAOFANYIKA TAREHE 16 DISEMBA, 2020

Tafadhali rejea mada tajwa hapo juu,

2. Kwa mujibu wa mwongozo wenye Kumb. Na.AB.110/215/01/31 wa tarehe 17 Novemba, 2020 unaohusu taratibu za kuendesha Mkutano wa kwanza wa Halmashauri, kumchagua Meya/Mwenyekiti na kuunda Kamati za Kudumu za Halmashauri ukisomwa pamoja na Kanuni ya Kudumu za Halmashauri ya Jiji la Dar-es-salaam za mwaka 2014 kifungu 3 (1) (a) unaeleza kuwa mara baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutangaza matokeo ya uchaguzi wa Madiwani wa Kata na Uteuzi wa Madiwani wa Viti maalum, Mkurugenzi wa Halmashauri ataitisha Mkutano wa Kwanza wa Madiwani wote wa Dar-es-salaam ili uweze kumchagua Meya au Mwenyekiti, Naibu Meya au Makamu Mwenyekiti na wajumbe wa Kamati za Kudumu za Halmashauri.
3. Kwa maelezo yaliyotangulia, ninatoa taarifa rasmi kuwa tarehe 16/12/2020 utafanyika Mkutano wa Madiwani wote wa Manispaa za Dar-es-salaam kwa ajili ya uchaguzi wa kumchagua Meya wa Jiji la Dar-es-salaam.
4. Mkutano huo utafanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Karimjee (Main Hall) kuanzia saa 3:30 Asubuhi.
5. Tafadhali mnaombwa kuhudhuria bila kukosa na kwa kuzingatia muda uliopangwa.

**NB:** Barua hii inafuta barua yenye Kumb. Na. AB.50/75/01/64 ya tarehe 04 Disemba, 2020.

Sipora J. Liana,

**MKURUGENZI WA JIJI.**